# MwanaHisa

CRDB BANK PLC

Toleo la Juni, 2015

Yaliyomo


- Faida Ya Benki Yakua Kwa Mwaka 2014 ........ 1
- Tangazo Kwa Wanahisa. ........ 2
- Ujue Waraka Mizania Wa Benki ........ 2
- Kukua Kwa Teknolojia Katika Tasnia Ya Benki Ni Fursa ........ 3
- Semina Kwa Umma Juu Ya Njia Mbalimbali Za Kukuza Mitaji ........ 4
- Mkutano Mkuu Wa Ishiriini Watoka Na Maazimio Makuu ........ 6
- Mkutano Mkuu wa 20 katika Picha. ........ 7
- Kibonzo. ........ 8


# FAIDA YA BENKI YAKUA KWA MWAKA 2014

Benki ya CRDB imezindua rasmi ripoti ya utendaji na Hesabu kwa Mwaka 2014, ambapo imefanikiwa kukuza faida kwa asilimia kumi na nne (14) ikilinganishwa na faida iliyopatikana mwaka 2013. Akiwasilisha taarifa hiyo katika Mkutano Mkuu wa Ishirini, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki, Dr. Charles Kimei, alieleza sababu za ukuaji wa faida ni kutokana na kukua kwa mapato yatokanayo na huduma zitolewazo na Benki. Hii imetokana na utekelezaji wa mkakati wa biashara wa miaka mitano, ambao unalenga kuongeza ufanisi katika kuboresha huduma mbalimbali kwa wateja, kupunguza gharama za uendeshaji na upanuzi wa mtandao wa Benki nchi nzima.




*Mwenyekiti wa Bodi Bw. Martin Jonas Mmari akiwasilisha ripoti ya Wakurugenzi kwenye Mkutano Mkuu wa Ishirini Jijini Arusha tarehe 9 Mei, 2015*

Pamoja na ukuaji wa faida, Benki pia imefanikiwa kukuza thamani ya rasilimali, amana, mikopo na fedha za wanahisa na hivyo kuendelea kuongoza katika soko la huduma za kifedha. Akifafanua zaidi, Mkurugenzi Mtendaji alielezea ukuaji katika maeneo hayo ni kama ifuatavyo:

- Amana ziliongezeka kwa asilimia 12 kutoka shilingi bilioni 3,024 kwa mwaka 2013 hadi kufikia shilingi bilioni 3,391 kwa mwaka 2014.
- Mikopo iliongezeka kwa asilimia 28 kutoka shilingi bilioni 1,993 mwaka 2013 hadi kufikia shilingi bilioni 2,545 mwaka 2014.

**ANUANI**
Mhariri Mwanahisa
CRDB Bank Plc
Office Accomodation scheme
Mtaa wa Azikiwe, Ghorofa ya 4
S.L.P. 268
Dar es Salaam

Simu Na: 002 - 2117442 - 7
2114237
Fax No. 022 - 2131005
Barua pepe:
investorrelations@crdbbank.com
Tovuti: www.crdbbank.com

**MAONI KUTOKA KWA MWANAHISA**

Wanahisa wanapewa fursa ya kufikisha maoni, ujumbe au mapendekezo katika jarida hili kwa kutumia anuani inayoonekana hapo juu.

- Rasilimali ziliongezeka kwa asilimia 19 kutoka shilingi bilioni 3,558 kwa mwaka 2013 hadi kufikia shilingi bilioni 4,223 kwa mwaka 2014.
- Fedha za Wanahisa (*Shareholders Funds*) ziliongezeka kwa asilimia 17 kutoka shilingi bilioni 375 mwaka 2013 hadi kufikia shilingi bilioni 441 kwa mwaka 2014.
- Faida ya Benki imekua kwa asilimia 14 kutoka shilingi bilioni 84 mwaka 2013 hadi kufikia shilingi bilioni 96 mwaka 2014.

## *Tangazo kwa Wanahisa Wote*

Mpendwa Mwanahisa, unakumbushwa endapo hujalipwa gawio lako, tafadhali fika katika tawi lolote la Benki ya CRDB, ili uchukue malipo ya gawio lako kwa miaka ifuatayo:

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **1996** | **1998** | **2000** | **2001** | **2002** | **2003** | **2004** | **2005** |
| **2006** | **2007** | **2008** | **2009** | **2010** | **2011** | **2012** | **2013** |

***Imetolewa na Katibu wa Bodi***

# Ujue Waraka Mizania wa Benki

Sheria inayoongoza uendeshaji katika sekta ya fedha na taasisi za kibenki ya mwaka 2006 (Banking and Financial Institutions Act 2006), inaagiza matokeo ya hesabu za Benki ya robo mwaka, kwa hesabu zisizokaguliwa na kila mwaka kwa hesabu zilizokaguliwa, kuwekwa wazi kwa umma na wanahisa, kwa kupitia njia mbalimbali kama vile magazeti, tovuti za Benki (www.crdbbank.com). Kila Mwanahisa anahimizwa kusoma magazeti na kutembelea tovuti ya Benki ili kusoma taarifa mbalimbali za Hesabu za kila mwisho wa robo mwaka na ripoti ya mwaka mara inapotolewa ili kujua utendaji wa Benki.

Hesabu za Benki zimegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni:

- Waraka Mizania (Balance Sheet/*Statement of Financial Position*);
- Taarifa ya Mapato na Matumizi (Income Statement/Profit & Loss Account/*Statement of Comprehensive Income*); na
- Taarifa ya Mtiririko wa Fedha (Statement of Cashflow).

Kama mtakukumbuka, katika toleo lililopita la Mwanahisa, tulianza kudadavua vipengele mbali mbali vya hesabu za Benki ili kumuwezesha kila mwanahisa kusoma na kuelewa kwa urahisi hesabu za robo mwaka na mwisho wa mwaka. Katika toleo hili, tutaendelea kudadavua moja ya sehemu muhimu ya Hesabu za Benki iitwayo **Waraka Mizania au kwa kiingereza Balance Sheet/Statement of Financial Position.**

## *Waraka Mizania ni nini?*

***Waraka Mizania*** ni taarifa ya kifedha inayotoa muhtasari wa Rasilimali, Madeni na Mtaji wa Benki katika kipindi maalumu. Taarifa hii huonyesha thamani ya rasilimali (assets) ambazo Benki inamiliki. Kwa mabenki, rasilimali kubwa ni mikopo iliyotolewa kwa wateja mbalimbali (watu na makampuni katika sekta binafsi na kwa serikali) pamoja na rasilimali zisizohamishika (fixed assets). Upande wa pili wa mizania unaonyesha Madeni (liabilities) zinazowakilishwa na Amana (deposits)

*Inaendelea uk 5*



CRDB BANK
The Bank that Listens

# Kukua kwa Teknolojia katika tasnia ya Benki ni Fursa

Maendeleo katika teknolojia ya mawasiliano (Tehama), yamechangia kwa kiasi kikubwa kubadilisha namna kampuni na taasisi zinavyofanya biashara na kutoa huduma, kwa kuboresha ubunifu katika bidhaa na ubora wa huduma.

Tunapozungumzia teknolojia katika tasnia ya benki inajumuisha vifaa na aina zote za mifumo inayowezesha kuwasiliana, kusambaza, kutunza, kutangaza na kubadilishana taarifa na kutoa huduma. Hii inajumuisha vitu kama radio, televisheni, video, simu, *computer*, "*network* hardware and software", vifaa, mashine na huduma zitokanazo na "TEHAMA" kama vile barua pepe, ujumbe wa simu za mkononi n.k.

Ukuaji wa kasi katika teknolojia ya mawasiliano, umeleta mapinduzi makubwa katika bidhaa na utoaji wa huduma za kibenki hapa nchini. Kwa sasa, matumizi sahihi ya teknolojia katika utoaji wa huduma za kibenki, imekuwa ni nyenzo muhimu ya kimkakati ili kukabiliana na ushindani. Benki zimeendelea kushindana kwa ubunifu wa bidhaa, kuongeza ufanisi kwa kupunguza gharama za uendeshaji na kuboresha huduma kwa wateja.

***"Ukuaji wa Tehama na matumizi yake katika utoaji wa huduma za kibenki, umewezesha wananchi kuunganishwa katika huduma rasmi za kibenki…hivyo kuongeza wateja wa benki"***

Matumizi ya Tehama yanaiwezesha benki kuwafikia wateja wengi zaidi na kwa gharama nafuu kwa kutumia njia mbadala za kutolea huduma tofauti na ilivyokuwa hapo awali (*traditional brick branches*).

***Makala hii itaendelea katika toleo lijalo la Mwanahisa, ambapo tutaainisha fursa mbalimbali zitokanazo na maendeleo ya teknolojia katika tasnia ya Benki. Katika makala ijayo tutabainisha fursa ambazo Mwanahisa anaweza kuzitumia ili kukuza kipato na kujiletea maendeleo. Tafadhali usikose nakala yako ya Mwanahisa toleo lijalo.***




*Mkurugenzi Mtendaji wa Benki, Dkt. Charles Kimei akikabidhi ufunguo wa gari kwa Mshindi wa kwanza wa gari aina ya Passo katika promosheni ya Shinda Passo Bi. Tumaini Mwakajwanga. Promosheni hii bado inaendelea nchi nzima ili kuhamasisha matumizi ya huduma ya Simbanking kwa wateja wa Benki. Huduma ya Simbanking ni moja ya kielelezo cha fursa zinazotokana na kukua kwa matumizi ya Tehama.*

# Semina Kwa Umma Juu ya Njia Mbalimbali za Kukuza Mitaji

Benki ya CRDB hivi karibuni, imeendesha semina nchi nzima, Tanzania bara na Zanzibar ili kuelimisha umma juu ya fursa mbalimbali za kukuza Mtaji kwa Kampuni zilizoorodheshwa katika soko la hisa.

Akifungua semina hiyo, katika kituo cha Hotel ya Peacock mjini Dar es salaam, Mkurugenzi wa tawi la Lumumba, Bwana John Almasy alisema, huu ni utaratibu ambao Benki imejiwekea kila mwaka, ambapo huendesha semina nchi nzima ili kuelimisha umma juu ya masuala mbalimbali ya ki-uchumi.

Usemi wa Kiswahili usemao, "Umoja ni Nguvu Utengano ni Udhaifu", ulikuwa dhahiri katika mada hii. Kwani mtoa mada Mkurugenzi wa tawi la Vijana, Bwana Pelesi Fungo, aliainisha kwa kina dhana ya kukuza mtaji kwa kupitia Dirisha Kuu (MIM) na Dirisha Dogo (EGM) za Soko la Hisa Dar es Salaam (Dar es Salaam Stock Exchange).

Akitoa ufafanuzi, mtoa mada alisema, utaratibu wa kukuza mtaji kupitia dirisa dogo ni fursa pekee inayoruhusu wajasiriamali wadogo wadogo, wasiokuwa na historia ya biashara kujipatia mtaji kupitia soko la hisa la Dar es Salaam. Kwa kujiunga pamoja, wakiwa na wazo la biashara, watanzania wanaweza kutumia dirisha dogo ili kupata mtaji ili kuendesha shughuli za kiuchumi.

Pamoja na elimu iliyotolewa kupitia mada hizi, washiriki walipata fursa ya kuuliza maswali yaliyotokana na mada husika, pamoja na masuala mbalimbali ya Benki ya CRDB.

Akihitimisha semina hii mjini Arusha, Dk. Warsame alifafanua kwa kina njia nyingine ya kukuza mtaji kwa kampuni iliyoorodheswa katika soko la hisa kupitia utoaji wa Hisa Stahili. Huu ni utaratatibu ambao kampuni hutoa hisa kadhaa kwa wanahisa waliopo kwenye Daftari la Wanahisa hadi tarehe iliyoamriwa, ili kuwaruhusu kuzinunua. Mwaka huu, Benki ya CRDB imeamua kutoa Hisa Stahili ili kukuza mtaji wake na hivyo kuiwezesha kutekeleza matakwa ya kisheria ya mtaji na kugharimia miradi mbalimbali ya ukuaji wa Benki.




*Prof. Mohamed Warsame akiwasilisha mada mojawapo katika Semina ya Wanahisa wa Benki ya CRDB iliyofanyika Jijini Arusha tarehe 8 Mei, 2015, kuhusu Ukuzaji wa Mitaji kwa Kampuni zilizoorodheshwa katika soko la hisa.*



CRDB BANK
The Bank that Listens

*Inaendelea kutoka uk 2*

na madeni mengine pamoja na mtaji wa wanahisa (paid up capital) na limbikizo la faida (retained earning reserves). Pande mbili za mizania ni lazima zilingane, yaani;

**Assets (mikopo + rasilimali zisizohamishika na nyinginezo) = Liabilities (Madeni + Mtaji + Limbikizo la faida).**

Kwa maana hiyo, Benki ni kampuni inayowaunganisha wateja wa aina mbili: wanaoweka akiba kwa kupitia amana (deposits) na wale wenye mahitaji ya kuwekeza (wakopaji – borrowers). Kwa kukusanya amana ndogo ndogo na kubwa mahali pamoja, benki zinakuwa na uwezo wa kuwakopesha wateja wadogo wadogo, wa kati, makampuni makubwa na hata serikali za mitaaa na serikali kuu. Kwa kutekeleza wajibu huu, benki zinakuwa kichocheo kikubwa kwa ukuaji wa pato la taifa na katika kuleta maendeleo kwa ujumla. Uwekezaji hususani kwenye mikopo unaiwezesha benki kupata mapato ya riba ambayo kwa kawaida ni lazima yawe juu zaidi ya malipo ya riba kwa wanaoweka amana (depositors).

***Usikose toleo lijalo la Mwanahisa ambapo tutaelezea namna ya kusoma na kuelewa taarifa iliyomo katika waraka mizania wa Benki.***

# Je Wajua?

Kuwa Bodi ya Wakurugenzi wa CRDB Bank Plc, imepata kibali kutoka kwa Wanahisa katika Mkutano Mkuu wa ishirini uliofanyika jijini Arusha tarehe 9 Mei, 2015 ili kuendelea na utoaji wa Hisa Stahili? Kwa sasa, majadiliano yamekamilika kati ya Benki na wawekezaji ambao watashika nafasi ya udhamini wa hisa ambazo hazitachukuliwa.

Benki imeamua kuuza hisa za kawaida zipatazo 435,306,432 kwa Wanahisa watakaokuwepo kwenye rejista ya wanahisa hadi ifikapo tarehe 18 Juni 2015, kwa kiwango cha hisa moja (1) kwa kila hisa tano (5). Bei ya hisa hizo imepunguzwa kwa punguzo la asilimia 22 ya bei ya soko ya wastani wa siku 90 ili kuwawezesha wanahisa walio wengi kunufaika na utaratibu huu. Mchakato huu utakuwa tayari hadi ifikapo tarehe 22 Juni, 2015 ambapo kila mwanahisa atapatiwa barua ya allotment ambayo itaonyesha hisa alizonazo na hisa stahili ili aweze kuzinunua.

Uamuzi huu umefikiwa ili kuongeza mtaji wa Benki kukidhi matakwa ya kisheria ya mtaji kuendana na ukuaji wa Benki na pia kuiwezesha kutekeleza miradi mbalimbali inayolenga kupanua mtandao wake.

Mapato halisi yatakayotokana na utoaji wa hisa stahili, yatatumika katika kupanua mtandao wa Benki ya CRDB hapa nchini na katika kanda ya Afrika Mashariki, pamoja na kugharimia uwekezaji unataokiwa katika mifumo ya TEHAMA, ili kuendana na utekelezaji wa mpango mkakati wa Benki wa miaka mitano, na kukidhi matakwa ya Benki Kuu ya Mtaji.

Habari ndio hiyo, wanahisa wote mnahimizwa kutumia fursa hii kuongeza hisa zako kwa kununua hisa stahili na hivyo kuboresha umiliki na kiwango cha gawio kwa miaka ijayo. Mwanahisa anaweza kutumia fedha atakazopata kwenye gawio ili kununua hisa stahili au kukopa kutoka taasisi nyingine za fedha.

Endapo mwanahisa atashindwa kununua hisa zake, hisa hizo zitanunuliwa na mwekezaji mdhamini ambaye atamlipa mwanahisa thamani ambayo ni tofauti kati ya bei aliyonunulia yeye na bei ya mwanahisa. Malipo yanayotokana na manunuzi ya hisa stahili yatakayofanywa na mdhamini, yatatumwa kwa mwanahisa husika kwa utaratibu unaotumika kulipa gawio.

# Mkutano Mkuu wa Ishirini Watoka na Maazimio Makuu 5

Hivi karibuni Benki ya CRDB ilikuwa na Mkutano Mkuu wa **Ishirini mjini Arusha katika kituo cha Mikutano cha Kimataifa tarehe 9 Mei, 2015.** Mkutano huu ulitanguliwa na semina kwa wanahisa iliyofanyika tarehe 8 Mei, 2015. Semina hii ilikuwa na Mada kuu mbili ambazo ni: ***"Fursa zitokanazo na Huduma ya Uwakala wa Benki ya* CRDB**" na ***"Ukuzaji wa Mitaji kwa Kampuni zilizoorodheswa katika soko la hisa".*** Baada ya semina hii, jioni yake kulikuwa na hafla ya kukata na shoka iliyojumuisha wajumbe wote wa mkutano mkuu iliyokuwa imepambwa na burudani kibao!



*Mwanahisa akitoa maoni na kuuliza swali kwenye Mkutano Mkuu wa Ishirini wa Benki uliofanyika hivi karibuni Jijini Arusha.*

Mkutano wa ishirini ulikuwa ***muhimu sana*** kutokana na kuwa na ajenda muhimu kwa ustawi wa Benki mojawapo ikiwa ni kupitisha azimio la kuongeza mtaji. Dondoo nyingine za Mkutano huu zilikuwa ni: kufungua mkutano, kuchagua mwenyekiti na makamu mwenyekiti wa Mkutano Mkuu, Kuridhia ajenda ya Mkutano, Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu uliopita, Kujadili yatokanayo na kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa kumi na tisa, kujadili na kupokea taarifa ya bodi ya wakurugenzi na taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za mwaka 2014, kuidhinisha gawio kwa mwaka 2014, kuidhinisha ongezeko la mtaji kwa kutoa hisa stahili, kuidhinisha mapendekezo ya mabadiliko kwenye katiba ya Benki (Azimio Maalum), kuidhinisha ada ya wakurugenzi, kuteua wakaguzi wa hesabu, kuchagua wajumbe wa bodi, mengineyo kwa idhini ya mwenyekiti, kupanga mahali na tarehe ya mkutano ujao na kufunga mkutano.

Mkutano wa mwaka huu ulifana sana kwani ulihudhuriwa na wanahisa wengi ambao idadi yao ilikuwa zaidi ya elfu moja, waliowakilisha asilimia 75.6 ya hisa zote. Wanahisa hawa, walitoka sehemu mbalimbali za taifa letu na walikuwa wamejaa hamasa kubwa katika kutoa michango, mawazo na kuuliza maswali yaliyolenga kuboresha utendaji wa Benki na kuifanya iendelee kuongoza katika utoaji wa huduma bora za kifedha hapa nchini.

Siku ya mkutano ilitanguliwa na chai ya asubuhi kwa wajumbe wa mkutano. Mahudhurio yalikuwa mazuri pamoja na hali ya kujituma kutoka kwa wajumbe wote wa mkutano na hivyo kuwezesha maazimio muhimu 5 kufikiwa:

- Gawio kwa wanahisa la shillingi 15 kwa kila hisa.
- Kuongeza Mtaji wa Benki kwa kutoa Hisa Stahili moja (1) kwa kila hisa tano (5) za kawaida.
- Kupitisha malipo ya Wakurugenzi wa bodi kwa mwaka 2015.
- Uchaguzi wa Wajumbe wa bodi ambapo Bw. Juma Abdallah Abdulrahman na Bi. Devotha Ntuke Minzi walichaguliwa kuwakilisha wanahisa wenye hisa chini ya asilimia moja; na Bi. Rose Felix Metta alichaguliwa kuwa mjumbe wa bodi kuwakilisha wanahisa wenye hisa kati ya asilimia moja hadi kumi.
- Kuidhinisha mabadiliko katika katiba ya Benki ili kutambua wadhamini wa mchakato wa Hisa stahili na mpango wa kujitoa wa Danida Investment Fund (DIF).



CRDB BANK
The Bank that Listens

# Mkutano Mkuu wa 20 wa Benki Katika Picha




*Bi. Devota Ntuke Minzi akiwashukuru wanahisa mara baada ya kuchaguliwa kuwa mjumbe wa bodi kuwakilisha wanahisa wenye hisa chini ya asilimia moja (1)*




*Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa Ishirini Bw. Obeid Masajone akipokea zawadi kutoka kwa mwanahisa mara baada ya kumaliza kuongoza Mkutano Mkuu.*



*Mwenyekiti wa Bodi Bw. Martin Jonas Mmari akikabidhi zawadi ya pongezi kwa uongozi uliotukuka, kwa Balozi Mstaafu Damian David Ruhinda kwa kuongoza Mkutano Mkuu kwa kipindi cha miaka 15 mfululizo. Bodi pia ilikabidhi zawadi kwa Mwenyekiti Msaidizi Bi. Gatti Marwa, iliyopokelewa na mwanahisa aliyemteua kumwakilisha.*



*Pichani: Wanahisa wa Benki ya CRDB wakisikiliza kwa makini mada mbalimbali zilizowasilishwa katika Mkutano Mkuu wa Ishirini uliofanyika tarehe 9, Mei 2015 Jijini Arusha.*




*Pichani: Baadhi ya wanahisa, viongozi pamoja na baadhi ya wafanyakazi wa Benki wakijisajili tayari kuanza Mkutano Mkuu wa Ishirini siku ya Jumamosi tarehe 9 Mei, 2015.*



*Pichani: Wanahisa wakifuatilia mada zilizowasilishwa kwenye Semina ya wanahisa iliyofanyika tarehe 8 Mei, 2015 siku moja kabla ya Mkutano Mkuu. Mada hizo zilikuwa ni "Ukuzaji wa Mitaji kwa Kampuni zilizoorodheshwa katika soko la hisa" na "Fursa zitokanazo na Huduma ya uwakala wa Benki ya CRDB".*

# Kibonzo






CRDB BANK
The Bank that Listens